**DIOCESE DE KASONGO**
**SOEURS MISSIONNAIRES DE LA CROIX ET DE LA MISERICORDE ‘’ SMCM’’**
**Une famille religieuse au service des pauvres dans les périphéries**



# CEREMONIAL DES SMCM

**IBADA YA MISA**

**KIFUPI CHA MPANGO WA SIKU YA MUNGU**

1. Siku ya Mungu hiyo kutakua sherehe Kubwa, ambao:

Ma Binti ……. watakubaliwa kauanza mafundisho za kibikira katika shirika la Wamama wa Misionari wa Msalaba na Rehema y Mungu ndani ya jimbo la Kasongo.

Mabinti aawo wataanza **kipostilanti** na kupata mafunzo mabalimabli ya shirika lao: **watafanya atua moja mbele**. Watakuwa na mavazi kama alama itakao watambulisha popote kama Mabinti wanao jitayarisha kwa Maisha ya kitawa katika shirika hili. Pia watavikwa Medaille ya kitambulisho cha shirika hilo.

Ndio maana mwanzo wa ibada ya Misa tendo hilo litafanyika ili tuone sisi wote namna gani wataanza atua ya kwanza kwa kufikia siku moja kuitwa Ma Bikira.

2. Siku iyo ya Mungu kutakuwa pia kutoa **Maagano ya Milele** ya Wamama ……………….. (citez les noms des Soeurs) wataagana mpaka kufa kubaki katika Shirka la Wa Mamaa wa Misionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu.

Ndio maana kiisha hutuba, tutafuata maneno na matendo itakayo sindikiza Aagano hilo mbele ya Mung una mebel ya Ekyezia.

3. Siku ya leo pia kutakuwa Agano la Wakristu wa Shirika la Wamisionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu, wataagana kumtumikia Mungu kwa njia ya utumishi wa kutangaza Rehema ya Mungu popole wanapoishi na kushirikia kipaji cha jamaa ya Wamisionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu.

Ndio maana kiisha naziri ya milele ya Wamama, hufuata maagano ya Walaiki wa gundi hilo. Tutafuata aagano yao mbele ya Mung una mbele ya Eklezya.

**Utangulizi; Ibaba ya kutoa naziri ya milele**

Kwa desturi, ibada ya kutoa naziri ya Mielel ya Bikira, inaanza na Maandamano pamoja na yule ao wale watakao toa agano la Naziri, na kuelekea mbele ya altare.

Watakapo ingia katika mlango wa sifa: huimba wimbo wenye kuwa na maneno ifuatayo:

**Refrain; ‘’ Nimekuita uwe Mwangaza’’**

**Padri:** nimekuita uwe Mwangaa ili wokovu wangu ufike mpaka mipaka yote ya dunia.

**Bikira:** Bwana wangu mimi hapa niko tayari unigeuze niwe sura ya Rehema yako

**Padri**: Nimekufanya uwe mwangaza ili Rehema yangu inenee duniani kote

**Bikira**: Bwana wangu mimi hapa niko tayari, unisaidiye katika umaskini na uzaifu wangu, niweze kukujulisha na kukupendesha kwa watu wote

**Padri**: Nimekufanya uwe mwangaza ili utangaze ushindi wa shangwa ya mapendo yangu ulimwengu kote

**Bikira**: Bwana wangu mimi hapa, unipokee katika hesabu ya wale wanaotaka kutumikia ushindi wa shangwe ya mapendo yako duniani kote

Kisha kufika mbele ya altare na kuinama kwa heshima, watakao towa naziri wanarudi kuketi nafasi iliyo tayarishwa kwa ajili yao.

Wakati wa maandamano, kila yule anachukua mshumaa wenye kuwaka mikononi mwake, waimbaji wanaimba wimbo wa wito.

Ibada takatifu ya Misa inaanza kama desturi

**Ibada ya neno la Mungu**

Somo la kwanza: Is 49; 1-6

Zaburi: “Matendo ya huruma, ….’’

Somo la pili:

Enjili: Mt 5; 1-12 ou Jn 19, 25-27 ou Mt 25, 31- 40 ou Lc 4; 16-21.

NB. Lakini kama Ibada ya Naziri ufanyikasiku ya Mungu, nivema kulinda masomo ya siku ya Mungu kufatana na Ordo.

Par exemple 26e dimache du temps ordinaire “B’’

Nb: 11, 25-29; Ps; 18b; Jc 5, 1-6; Mc 1 38 -43.45. 47-48.

Hotuba

IBADA YA NAZIRI YA MILELE

Kiisha hotuba, ibada ya kutoa naziri ya milele inanza

Padri analika wale watakao toa naziri ya milele akitumia naneno aya

**Wajongee wale watakao fanya naziri**

Kila umoja anaitwa kwa jina lake na kujibia binafsi

"**Mimi hapa''**

**Mama ………………………………………….**

**Mama …………………………………………**

Watakao toa naziri ujielekeza mbele ya Askofu

Askofu ao mwakilishi wake anakaa katika kiti mbele ya altare

**MAZUNGUMUZO KATI YA ASKOFU NA BIKIRA**

**Askofu:** Unaomba nini kwa Eklyezi ya Mungu?

**Bikira:** Ninaomba kufanya naziri ya milele katika shirika la Mabikira wa Msalaba na Rehema ya Mungu

**Askofu:** Munajuwa kama kufanya agano la milele nikuwa tayari kujitolea na kuishi Maisha yenu yote mpaka kufa, kipaji cha pekee Roho Mtakatifu amewajalia jamaa ya Wamisionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu ndani ya Eklyezya.

**Askofu:** Ndiyo maana nawauliza mbele ya taifa la Mungu: muko tayari kutangaza Rehema ya Mungu kwa wadogo, wamaskini na wale walio achiliwa, mkisharikia magumu na furaha yaho?

**Bikira:** Kwa msaada wa Mungu, tuko tayari

Askofu: Mupo tayari kumtangaza, mumjulisha na kumpendesha Yesu Kristu kwa wale wasiyo mjua bado ili wokovu wake ufike mpaka mipaka ya dunia?

**Bikira**: Tukitumainia msaada wa Mungu, tupo tayari.

**Askofu:** Ukomo wa kitume ya jamaa yaw a Misionari wa Msalaba na wa Rehema ni kumpelekea Yesu mioyo.

Sasa nawauliza tena: mupo tayari kutoa Maisha yenu yote mkisali kwa ajili ya uongofu wa wakosefu wenyi zambi, kwa ajili ya roho za matoharani na kuichukua dunia nzima chini ya Msalaba wa Bwana?

**Bikira:** Tukitumainia Yesu Kristu aliyetupenda mpaka kutoa uzima wake kwa ajili yetu, tupo tayari.

**Askofu:** Wamisionari wa Msalaba na wa Rehema ya Mungu wanapokea kitume chao chini ya Msalaba karibu ya mama Maria.

Sasa nawauliza: muko tayari kuwapokea na kuwalinda waana wa Mungu wanaotangatanga na kuachiliwa katika usiku wa zambi, umaskini na kifo ili kuwaletea kitulizo na kuwarudishia matumaini?

**Bikira:** Tukisaidiwa na maombezi ya Mama Bikira Maria, Mama wa Eklyezya na Mama yetu, tupo tayari kuipokea kitume chetu chini ya Msalaba wa kutangaza katika sala, maneno na matendo yale tunayo tizama juu ya Msalaba, yaani Mapendo makubwa ya Mungu kwetu sisi na kwa ajili **ya ulimwengu mzima?**

**Askofu:** Basi Roho Mtakatifu akamilishe yale alionzisha ndani mwenu.

Kiisha hapo, huimba wimbo wa **"Roho Mtakatifu'**

**KUOMBA MSAADA WA WATAKATIFU WA MBINGU**

Kiisha Askofu anasimama, anapiga magoti kwa kuanza wimbo wa **litania.**

**Askofu**: Tukitumainia maombezi ya watakatifu wote, tuwatoleye ndugu zetu hawa ili waweze daima kufuata mifano………………………….

Huimba wimbo wa litania ya watakatifu

**KUTIA NAZIRI YA MILELE**

Hutayarisha Msalaba kwa Kufanya mahagano.

Askofu akiisha keti, anaalika Birikira kutia naziri. Juu ya meza ndogo mbele yake, anatia Msalaba na bitabu cha kanuni ya Shirika.

**Askofu:** Mwanangu, kwa kuwa unakusudia kujitolea kwa Mungu, tunakualika kutia naziri.

Bikira anafika kutia naziri. Anapo fika mbele ya Askofu, Bikira anapiga Magoti, anapiga alama ya Msalaba, anaanza kusoma kartasi, iliyo kuwa na maneno ya naziri akatia mkono wa kuume juu ya Msalaba na kitabu cha kanuni ya Shirika.

Bikira anapanda altareni kutia sahini yake juu ya kartasi.

Wakati wa kuita sahini, MAMA WA WOTE (Mère Générale), anasimamamia pembeni yake.

Kartasi inabakia altareni.

**MANENO YA MAAGANO YA MILELE**

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu**

**Kwa sifa na Utukufu wa Mungu, ili nitangaze huruma ya Mungu mahali popote,**

**Mimi…………………….. (jina), ninajinyenyekea chini ya Msalaba wa Bwana, mbele ya Akina Baba Askofu (Placide Lubamba ao Mwakilishi wake), na katika mikono ya Mama………………Mkubwa msimamizi wa shirika la Mabikira Wamisionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu, nagana na Kristu kuishi Maisha ya umaskini, usafi wa moyo na wa utii nikibaki karibu na wale wanaoachiliwa, kadiri ya sharia ya Mabikira wamisionaie wa Msalaba na Rehema ya Mungu.**

**Kwa hiyo nikitegemea maombezi ya Mama Maria, Mama wa Rehema, natoa Maisha yangu yote kwa Mungu.**

Hufuata teno la kusahihi katika kitabu cha Shirika (cf. Constitution, p31);

- Sahihi ya mtoa Naziri ya milele
- Sahihi ya Askofu ao Mwakilishi wake
- Sahihi ya Mama Mkubwa wa Shirika ao Mwakilishi wake.

**ALAMA YA UWAKIKISHO KWA KUKUBALIWA KATOKA SHIRIKA**

Kiisha kutia naziri;

Maman Mkubwa, atamuandika katika kitabu ya heshima ya Shirika. Na kutia sahihi pembeni ya jina lake, alama yenyi kuonesha kweli kama anakubaliwa katika shirika. Kiisha, Askofu ataweka sahihi yake.

Tena, MAMA WA WOTE atamkumbatya, alama ya kumtakia amani ndani ya Shirika lao kama mwana wa Shirika bila masito yoyote.

Na Askofu pia atamkumbatia.

**KUPASHA HABARI YA UWAKIKISHOKWA WAKRISTU**

**Askofu:** Ndugu wetu huyu anakuwa sasa Mnaziri wa milele, katika Jamaa ya Wamisionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu.

“Tunaweza kumpigia makofi ya shangwe’’

“wimbo moja wa wito’’

**MAHAGANO YA WALAIKI**

Kiisha naziri ya mielel ya Wamama, hufuta maagano ya Wakristue Wamisionari wa Msalaba na rehema ya Mungu.

Padri: Aanawahalika akisema:

Wajoingeye wale watakao fanya Agano lao la Umisionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu

**Mama ……………………………………….**

**Baba ………………………………………….**

**Padri**: Munaomba nini Kwa Eklezya ya Mungu?

**Mkirstu:** Tunaomba Kwa Eklezya ya Mungu, kukubaliwa kufanya Agano ya Kuwa watumishi wa Rehema ya Mungu popote tunapoishi duniani tukisharikia kitume cha jamaa ya Wamisionari wa Msalaba na Rehema.

**Padri**: Padri anajielekeza kwa Mama Mbubwa wa Jamaa ya Wamisionari wa Msalaba na Rehema na kumuliza:

**Akina Mama**, unahuakika kama ndugu zetu hawa …………………………. na ………………………… wapo tayari kuagana na Kristu mbele ya Eklzya ili iwa hakikishe kuwa wajumbe wa Rehema ya Mungu, wakisharikiana na jamaa ya Wamisionari wa Msalaba na Rehema?

**Mama Mkubwa**: kwa Rehema ya Mungu, na kisha kuchunguza vizuri Maisha yao ya kikristu ndani ya Eklezya na majitoleo yao kwa kutangaza rehema ya Mungu kwa njia ya sala, na matendo ya huruma, nina hakikisha kama wapo tayari.

**Padri**: Ndugu wapenzi …………………….. na ……………………………, Eklezya mama yetu inayo furaha ya kuhakikisha wito wenu kama Walaiki Misionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu, kwa hiyo kila moya wenu afanye Agano lake Mbele ya Mung una Mbele ya Eklezya.

**MAAGANO**

***Kajina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu,***

***Kwa ajili ya sifa ya Mungu, Mimi ………………… (jina), nanyenyekea chini ya Msalaba Mtukufu wa Bwana, na mbele ya Eklezya, na ahidia Kristu kuitangaza Rehema ya Mungu popote ninapoishi duniani nikishirikia Fazila ya jamaa ya Wamisionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu, yaani kutangaza huruma ya Mungu nikitenda matendo ya huruma ya kimwili na matendo ya huruma ya kiroho hasa kwa wale walio wadogo na wanao achiliwa.***

***Kwa hiyo naweka matumaini yangu kwa Yesu Kristu na namuomba anilinde kama vile yule anayepashwa kutumikia sifa yake isiyo na mipaka.***

***Baada ya Agano Walaiki wanapokea Msalaba***

***Kiisha uimba wimbo wa “Sifa kwa heshima ya Rehema ya Mungu’’***

***Kisha wana panda altereni, wanatia sahihi ku kartasi ya Agano.***

***Mama Mbukwa naye usahini***

***Padri naye usaini.***

Misa inaendelea kama desturi (KIPINDI CHA MATOELO).

# KIPINDI CHA PILI

# IBADA YA KUFUNGUA NOVISIATI

## JESUIBADA YA NENO LA MUNGU

*Yote yakiwa tayari, maandamano ya kuingia nyumbani mwa Mungu kwenda altareni yanapangwa kama desturi. Shemasi mmoja mwenye kuchukua kitabu cha Enjili anatangulia, mbele yake akiwa msindikizi mwenyi kuchukuwa chetezo yenye kutowa moshi wa ubani; mabinti watakaoingia katika kipindi ya kipostulanti na novisiati wanamfuata, nyuma yao Mapadri watakaotolea sadaka ya Misa pamoja na Askofu wanafuata; mwisho anakuja Askofu.*

*Wakati huo huimba Wimbo wa Kuingia, k.m.:*

Mtu akitaka kuitumikia, anifuate, asema Bwana; na pale nilipo, mtumishi wangu pia atakuwapo.
*Ao: (kwa mapadri)* *Luka 4, 18*
Roho ya Bwana juu yangu,
Kwa sababu amenipaka mafuta;
Amenituma niwahubiri maskini Habari Njema,
Kuwaponya walivunjika moyo.

## I. KUFUNGUA NOVISIATI

*Kisha usomi wa Enjili takatifu na hotuba ya Akina Baba Askofu, huanza hatua ya kufungua Novisiati. Inafanyika namna hiyo:*

- *Kwanza Padri mwongizi wa kiroho wa Shirika la mabikira wa Misionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu, anasoma barua ya kufungua Novisiati ya Mama msimamizi mkuu wa shirika.*
- *Kisha Padri mwengine anasoma Burua ya Akina Baba Askofu ya kutoa ruhusa ya kufungua Novisiati.*
- *Kisha wanawaalika Waamini kushangilia*.

## II. IBADA YA KUINGIA KATIKA KIPINDI CHA KIPOSTULANTI

### *II.1. KUWAITA WATAKAO INGIA KATIKA KIPINDI CHA KIPOSTULANTI*

*Bikira mmoja ao Padri mwongizi wa kiroho wa Shirika anaalika wale watakaoingia katika kipindi ya kipostulanti*:

**Wajongee wale watakao ingia katika kipindi cha kipostulanti**:

*Kila mmoja anaitwa kwa jina lake na kujibia binafsi*:

« **Mimi hapa** »

### *II.2. MAZUNGUMUZO*

*Watakao anza kipindi ya kipostulanti ujielekeza mbele ya Mama msimamizi wa jamaa ya mabikira wa Misionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu.*

*Mama msimamizi ao mwakilishi wake anasimama mbele. Na hapo mazungumzo kati ya Mama msimamizi ao mwakilishi wake na wapostulanti*

**Mama msimamizi**: munaomba nini kwa Jamaa ya mabikira wa Misionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu?

**Postulanti**: Nikijibu kwa mapendo ya Kristu aliyeniita nimfuate, ninaomba nikubaliwe kuanza mazoezi ya maisha ya kitawa kama postulanti katika shirika ya mabikira wa Misionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu.

**Mama msimamizi:** muko tayari kuchagua fungo lililo bora, yaani kuacha vyote, kumsilikiza Kristu Bwana na Mwalimu atakaye wafumbulia siri ya maisha ya kitawa kupitia mazoezi na maongozi ya wakubwa wenu?

**Postulanti:** Nikitegemea mapendo ya Kristu anayeniita niwe wake ili anigeuze niwe mjumbe wa Msalaba na Rehema yake, niko tayari.

**Mama msimamizi:** Mukitaka kwa uhuru wote kumfuata Kristu katika maisha ya usafi wa moyo, umaskini, utii na kujiachilia kuongozwa naye mkisharikia maisha ya kijamii ya mabikira wa Msalaba na Rehema ya Mungu, mufanye hatua moja mbele.

*Wapostulanti wanafanya hatua, kiisha wanasema maneno hayo:*

Ninaiacha dunia na umaridadi wake ili nimfuate Kristu, Bwana na Mwokozi wangu.

**Mama msimamizi**

- Mungu mwenyewe akamilishe yale aliyoanzisha ndani mwenu.

### *II.3. WIMBO*

*Wapostulanti wanaimba: Nimefanya hatua kiisha wanaimba*

Kiitikio

Nimefanya hatua niwe mjumbe wa Msalaba na Rehema (yako)

1. Uliwaita wamitume wakufuate, namimi pia ninafuata rehema yako.
   Mapendo yako Bwana wangu haina mwisho, unishike mkono Bwana usiniachilie.

2. Petro, Andrea, Yakobo na Yoane waliacha nyavu zao nao wakavua watu;
   Mwokozi wangu nami nitaacha vyote, ntakufuata wewe nasikia sauti yako.

3. Safari hiyo peke yangu sitaweza, uwe ngome langu tena uwe ngao langu.
   Penyi milima Bwana upa sawanyishe, penyi mabonde Bwana wangu upajaze.

### *II.4. KUWAVIKA MAVAZI*

*Mavazi watakao vikwa wapostulanti, inaletwa mbele ya Akina Baba Aksofu, naye anaibariki kwa sala hii:*

**Mama msimamizi:** mtapokea vazi mpya alama inaonyesha kama kwa wito wenu mnaishi kwa namna yapekee neema ya ubatizo. Mnamuvaa Kristu ukingo wenu na mpendwa wenu. Yeye anawaumba wapya ili muwe wake na awageuze kuwa sura hai ya Rehema yake.

*Kisha Akina Baba Askofu anabarikia mavazi*

***Askofu: Tunakuomba Ee Bwana, ubariki mavazi hii watakao vikwa mabinti hawa, watakapo ivikwa, wajaliwe neema ya kutambua kama wemevikwa mavazi ya wokovo na pia wamemvaa Kristu Bwana; ivi mwendo wao uonekane kuwa mwendo wa waana wamwanga. Kwa ajili ya Kristu Bwana wetu. Amen***

*Kisha Akina Baba Askofu ananyunyuzia mavazi maji ya Baraka.*

*MAMA msimamizi anawaganyia mavazi wote hujielekeza nafasi iliyo tayarishwa na wanavikwa mavazi. Kisha wanaingia kanisani wakisindizwa na wimbo, wakifika mbele ya altare wote anabusu na wanarudi panafasi yao.*

## III. KUINGIA KU NOVISIATI

### *III.1. KUWAITA WATAKAO INGIA KU NOVISIATI*

*Bikira mmoja ao Padri mwongizi wa kiroho wa Shirika anaalika wale watakaoingia ku Novisiati*:

**Wajongee wale watakao ingia ku novisiati**

*Kila mmoja anaitwa kwa jina lake na kujibia binafsi*:

« **Mimi hapa** »

### *III.2. MAZUNGUMUZO*

*Watakao anza kipindi ya novisiati ujielekeza mbele ya Mama msimamizi mkuu wa shirika ya mabikira wa Misionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu.*

*Mama msimamizi ao mwakilishi wake anasimama mbele. Na hapo huanza mazungumuzo kati ya Mama msimamizi ao mwakilishi wake na wanovisi.*

**Mama msimamizi**: Kiisha kusharikia muda wa miaka michache maisha ya kijamii pamoja nasi, muliomba kwa uhuru wenu kuanza novisiati. Sasa ninawauliza munangoja nini kwa Jamaa ya mabikira wa Misionairi wa Msalaba na Rehema ya Mungu?

**Postulanti:** Tunamshukuru Mungu, yeye Baba wa Rehema anayetuita kumfuata Kristu katika maisha ya kitawa ndani ya Jamaa ya mabikira wa Msalaba na Rehema ya Mungu. Ndio maana tunaomba kwa shirika letu:

- Mutufundishe kumfuata Kristu mpaka msalabani, tukiwa waaminifu kwa maisha ya sala na ya kujikatalia;
- Mutusaidie tumjue Yesu Kristu, tumjulishe na tumpendezeshe tukijifanya watumishi wa wote;
- Mutufundishe kuipenda Eklezya, kuitumikia na kutumikia ndugu zetu hasa wale wanaoishi mbali na wadogo wanaoachiliwa;
- Mutusaidie kuishi Enjili na kushika kanuni ya Shirika ya mabikira wa Msalaba na Rehema ya Mungu.

### III.3. KUPOKEA ALMA YA JAMAA YA MABIKIRA WA MISIONARI MSALABA NA REHEMA YA MUNGU

**Mama msimamizi:** Wadada wapenzi, munapoingia katika kipindi ya novisiati munaanza maisha ndani ya Jamaa ya mabikira wa Msalaba na Rehema ya Mungu. Ndio maana mutapokea alama mbali mbali inayo onyesha kama munatayarishwa kwa maisha ya kitawa ndani ya Jamaa hiyo: mutapokea mavazi ya pekee, mutavaa shela, mutavaa picha ya Yesu Mwenyi huruma na mutapokea jina mpya.

*Maalama watakao pawa wano, inaletwa mbele ya Akina Baba Aksofu, naye anaibariki kwa sala hii:*

**Ee Bwana Mungu wetu, unajaza viumbe vyako vyote baraka yako, usikilize sala ya watumishi wako watakao tumia alama hii ya shirika ya mabikira wa misionari wa msalaba na rehema ya Mungu, ndio mavazi, shela na picha ya Yesu mwenyi huruma: watakapo tumia alama hizi wajaribu kulinda amri zako na kupata vyote vinavyoweza kuwasaidia katika maisha ya kukufuata Wewe na kuendelea vema mpaka uzima wa milele. Kwa ajili ya Kristu, Bwana wetu. Amen**

*Kisha Akina Baba Askofu ananyunyuzia mavazi maji ya Baraka.*

**Mama msimamizi** anatoa maana ya alama zile mbalimbali

- **Mavazi na shela**: Mavazi ya pekee na shela inaonyesha kama kwa wito wenu mume wekwa kwake Bwana Yesu Kristu,
- **Picha ya Yesu mwenyi huruma**: Agizo la Bwana wetu Yesu Kristu kwa mtakatifu Faustina ni hayo: « Yeyote atakae ishi chini ya ulinzi wa Rehema yangu atapata ukingo ». Kwa hiyo, maji na damu inayotiririka kutoka Moyo wa Yesu kama chemchem ya Huruma kwa ajili yetu, iwakinge, iwatakase na iwape nguvu ya kumshuhudia ili kwa njia yenu, Rehema ya Mungu ienee duniani kote.

*Kisha wanovisi wanavikwa mavazi na shela*

### *III.4. BARAKA*

*Bikira mmoja ao Padri mwongizi wa kiroho wa Shirika anaalika wapostulanti wajiunge na wanovisi wakijongea mbele wapokee baraka.*

*Wote wanajiweka mbele ya Baba Askofu, wanapiga magoti.*

**Askofu: Ndugu wapenzi tumwombe Mungu, Baba mwenyezi, awabarikie kwa neema yake mabinti wake hawa, wanaotamani kumfuata Kristu katika shirika ya mabikira wa missionary wa msalaba na Rehema ya Mungu.**

*Kisha Akina Baba Askofu anatowa sala hii:*

**Ee Bwana unaye waita watumishiwako kwa utakatifu,**

**Uwafumbulie mapendo yako mabinti wako hawa, wanaotamani kuingia katika jamaa ya mabikira wa misionari wa Msalaba na Rehema ya Mungu. Uwajaze na neema yako ili wakiishi maisha ya kijamii na kufuata mafundisho ya Eklezya, watambue kwa msaada wa Roho Mtakatifu maana ya wito wao. Neema yako ee Bwana iwageuze kuwa Rehema ili nafsi yao yote ishuhudie Rehema yako. Kwa ajili ya Kristu Bwana wetu. AMEN**

### *III.5. WIMBO*

*Wapostulanti na wanovisi wanajielekeza ndani ya sakristia.*

*Bikira mmoja ao Padri mwongizi wa kiroho wa Shirika anawaalika waimbaji kuimba wimbo wa wito.*

*Wapostulanti na wanovisi wanaingia wakiimba wimbo huu:*

**WIMBO WA KUINGIA: NINAKUJA**

**Kiitikio:**

Ninakuja, kwako ee Bwana Yesu. Unifanye (niwe) mjumbe wa Msalaba na Rehema yako.

1. Nimesikia sauti yako imeniita. TS; Bwana wangu unipokee
   Umeniita kama vile Nabii Musa.TS; Bwana wangu unipokee
   Kuwakomboa waisraeli utumwani TS; Bwana wangu unipokee
   Walipokua utumwani mwa wa Misri. TS: Bwana wagu unipokee.
2. Nimesikia sauti yako imeniita. TS; Bwana wangu unipokee

*Wapostulanti wanaketi pa nafasi yao na wanovisi wanajielekeza mbele ya Mama msimamizi ili kupokea jina mpya.*

**III.6. KUWAPA JINA MPIA**

**Mama msimamizi**: kupewa jina mpya kunaonyesha mabadiriko ya maisha yenu na mamlaka munayopokea mbele ya Mungu.

*kila munovisi anapita mbele ya Mama msimamizi kupokea jina mpya*

**Mama msimamizi:** Dada Fulani … tangu leo utaitwa bikira hama sœur ….

*Na kiisha wanavikwa sura ya Yesu mwenyi huruma.*

*Wanovisi wanaimba wimbo ufwatayo*:

**YESU WANGU MWOKOZI WANGU**

**Kiitikio**:

Yesu wangu Mwokozi wangu: TS / Ninakushukuru Bwana wangu

Kwa kunifanya niwe wako: TS / Ninakushukuru Bwana wangu

Niko tayari kujiachilia: TS / Ninakushukuru Bwana wangu

Niongozwe nawe mwokozi: TS / Ninakushukuru Bwana wangu

1. Niko tayari kujitolea kwako
   Ili niongozwe nawe Mwokozi wangu
   Umenivika mavazi yako ya kitawa ee Bwana
   Nami niwe alama ya Rehema yako.

2. Nimesikia sauti yako ee Bwana
   Ginsi ulivyowaita wamitume wako
   Waitangaze Enjili yako duniani kote

Niko tayari Bwana wangu unitume.

*Bikira mmoja ao Padri mwongizi wa kiroho wa Shirika wapostulanti wajongee, kiisha wote pamoja na wanovisi wanasali sala hii*:

**SALA: Eee Yesu wangu, unichunge pembeni yako, na usiruhusu nijitenge nawe; angalia uzaifu wangu, bila Wewe siwezi kufanya hata hatua moja. Eee Yesu, inafaa basi, uwe daima pamoja nami kama vile mama asiyeacha mtoto wake mchanga, na hata zaidi ya ile, yeye akimwacha, ninayo matumaini kamili, wewe hautaniacha kamwe. Yesu ninakuaminia. Amen**

***KIISHA WANARUDI PA NAFASI YAO NAMISA INAENDELEA NA KIPINDI CHA KUSADIKI.***